KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

DIVISHENI YA KAZI

MASJALA NDOGO - ARUSHA

MAOMBI YA MAREJEO NA. 24 YA 2020

(Yanayotokana na Shauri la Mgogoro wa Kazi Namba CMA/ARS/ARB/104/2018)

BAINA YA

ALAF LIMITED .....MLETA MAOMBI

DHIDI YA

JIMMYTONNIE JOHN USIRI.....MJIBU MAOMBI

HUKUMU

11/8/2021 & 22/9/2021

ROBERT, J:-

Katika maombi haya, mleta maombi, ALAF LIMITED, anaiomba mahakama kufanya marejeo kwenye uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika Shauri la Mgogoro wa Kazi Na: CMA/ARS/ARB/104/2018. Katika Shauri hilo, Tume iliamua kuwa Mjibu Maombi alifukuzwa kazi isivyo halali kwa kuwa Mleta Maombi alishindwa kuonyesha kama zilikuwepo sababu za msingi za kumwachisha kazi Mjibu Maombi. Aidha, Tume iliona kuwa Mleta Maombi hakufuata taratibu za kisheria katika kumfukuza kazi Mjibu Maombi. Hivyo basi, Tume ilitoa tuzo ya Shilingi 19,800,000/= kama fidia kwa Mjibu Maombi kwa kufukuzwa kazi isivyo

halali. Mleta Maombi hakuridhishwa na uamuzi wa Tume na hivyo ameleta maombi haya akiiomba Mahakama kufanya marejeo katika uamuzi wa Tume, kuweka kando uamuzi huo na kutamka kuwa Mjibu Maombi alifukuzwa kazi kihalali.

Kwa ufupi, usuli wa shauri hili unaonyesha kuwa Mjibu Maombi aliajiriwa na Mleta Maombi mwaka 2009 kama Mhasibu na Meneja (Accountant and branch manager). Tarehe 19/12/2019, Mjibu Maombi aliachishwa kazi na Mleta Maombi kwa maelezo kuwa alitumia vibaya madaraka yake na kuisababishia kampuni hasara ya Shilingi 424,120,099/=. Mjibu maombi hakuridhika na uamuzi wa kuachishwa kazi na hivyo alipeleka lalamiko lake mbele ya Tume akitaka kulipwa fidia kwa kuachishwa kazi isivyo halali pamoja na malipo na stahiki zake mbalimbali za kikazi.

Tume katika kutoa maamuzi yake ilijiridhisha kuwa Mleta Maombi alishindwa kuthibitisha kuwa alimfukuza kazi Mjibu Maombi ilivyo halali na hivyo kutoa tuzo ya Shilingi 21,936,538/= ikiwa ni fidia ya mishahara ya miezi thelathini na sita (36) sawa Tshs. 19,800,000/=, notisi sawa na Shilingi 550,000/=, Kiinua mgongo kwa muda wa miaka saba (7) toka November, 2011 hadi tarehe 3/2/2018 sawa na Shilingi 1,036,538/= na likizo ya mwaka sawa na Shilingi 550,000/=. Mleta Maombi hakuridhishwa

na uamuzi huo, hivyo ameleta maombi haya ya marejeo kwa sababu zifuatazo;

a. Uamuzi wa Tume unakinzana na matokeo ya ushahidi uliofikishwa mbele ya Tume na kukiuka sheria.

b. Muamuzi alikosea kwa kutoa uamuzi usio halali na sahihi kuwa Mjibu Maombi aliachishwa kazi isivyo halali.

c. Muamuzi alikosea kwa kutoa uamuzi usio halali na sahihi kuwa Mjibu Maombi anastahili kulipwa fidia baada ya mkataba wake kuvunjwa pasipo taratibu za kisheria kufuatawa.

d. Tume ilienda kinyume na sheria katika kutekeleza mamlaka yake.

e. Kuwepo kwa makosa ya msingi katika mwenendo wa kesi mbele ya Tume na hivyo kusababisha kutolewa kwa uamuzi usiokuwa na haki kwa Mleta Maombi.

f. Muamuzi alitumia vibaya mamlaka yake.

g. Muamuzi aliendesha vibaya mwenendo wa shauri ili kutoa maamuzi aliyoyakusudia.

h. Katika kufanya uamuzi wake, Tume ilizingatia mambo ambayo hayakutajwa katika hati za shauri husika, mwendendo wa shauri husika au ushahidi uliotolewa katika Tume.

i. Kwamba, uamuzi wa Tume unapingana na matokeo ya ushahidi uliotolewa katika shauri husika.

Maombi haya yaliambatana na hati za viapo za: Prem Narayan Verma, Meneja wa Fedha (Financial Manager) wa Mleta Maombi; Meshack Christopher Mgeyekwa, Mhasibu (Management Accountant) wa Mleta Maombi; Richard Makoye Ndama, Afisa Rasilimali Watu (Human Resource Manager) wa Mleta Maombi na Adrian George Sigalla, (Senior Administrative Manager) wa Mleta Maombi na kupingwa na hati ya kiapo kinzani cha Mjibu Maombi.

Katika maombi haya Mleta Maombi aliwakilishwa na Wakili **Hamida Sheick** na upande wa Mjibu Maombi uliwakilishwa na wakili **Miriam Nitume**. Usikilizwaji wa maombi haya ulifanyika kwa njia ya hoja za maandishi kama ilivyoagizwa na mahakama.

Akifafanua sababu za maombi haya, Wakili wa Mleta Maombi aliieleza mahakama kuwa Mleta Maombi alimuachisha kazi Mjibu Maombi akiwa na sababu za msingi na alifuata taratibu zote za kisheria. Hivyo Tume ilikosea kusema Mjibu Maombi aliachishwa kazi bila sababu za msingi na pasipo kufuata taratibu za kisheria.

Akizungumzia kwa pamoja sababu zilizoainishwa katika vipengele (a), (b) na (e) vya sababu zake, Wakili aliielezea mahakama kuwa, Tume ilikosea kuamua kuwa DW3 (Richard makoye), hakuhudhuria kikao cha nidhamu wakati alihudhuria na jina lake lipo kwenye muhtasari wa kikao

kuwa ndiye aliyekuwa katibu wa kikao. Alifafanua zaidi kuwa jambo hili linathibitishwa na ushahidi wa Richard Mkoye Mwenyewe na Adrian Sigalla Pamoja na kielelezo D19 na D21 (Hearing form and Minutes of Disciplinary Committee), hivyo inashangaza kuona tume ikisema kuwa Dw3 hakuhudhulia kamati ya nidhamu.

Aidha, alifafanua kuwa Tume haikutilia maanani Ushahidi wa Dw4 (Clement Mlanda) ambaye alikuwa shahidi wa msingi kwenye shauri hili. Alitaja mambo ya msingi katika ushahidi wake ambayo hayakuzingatiwa na Tume kuwa ni pamoja na kuwa alinunua bidhaa kutoka kampuni ya ALAF tawi la Mwanza na kuleta katika kampuni yake (Mlashi General Traders Limited) iliyopo Baridi na kuwa asingeweza kununua bidhaa kutoka Arusha na kuzisafirisha hadi Bariadi kwasababu ya umbali. Aidha alitoa ushahidi kuwa hajawahi kusafiri kwenda India, hajawahi kuugua ugonjwa wowote mkubwa na hajawahi kufanya biashara yoyote na Mjibu Maombi. Haya yote ni mambo muhimu yanayothibitisha kuwa Mjibu maombi alimdanganya mwajiri wake.

Alieleza zaidi kuwa ushahidi wa DW5 ulibainisha kuwa Mjibu Maombi hakufukuzwa kazi kwa kutokuhudhuria kazini au kwa kumiliki kampuni yake binafsi (Ngosero General Supplies Limited). Alifafanua kuwa tatizo halisi na kampuni hiyo ni kuwa Mjibu Maombi bila kumtaarifu

Mwajiri wake alitumia nafasi yake kama Mhasibu wa tawi la Arusha na Afisa Mauzo kuipatia kampuni yake bidhaa kwa mkopo wakati akijua kuwa bidhaa hazikutakiwa kutolewa kwa mkopo isipokuwa kama mteja atakuwa na hadhi ya *dealer* (dealer status). Bidhaa ambazo Mjibu Maombi aliikopesha kampuni yake hazikuweza kulipiwa na kumsababishia hasara mwajiri wake ya Shilingi 320,658,999/= jambo ambalo halikuzingatiwa na Tume. Alibainisha pia kuwa, kitendo cha Mjibu Maombi kuchukua bidhaa kutoka kwa Mwajiri wake kwenda kwenye kampuni yake binafsi kilikuwa sawa na kitendo cha wizi na kilitosha kuwa sababu ya kufukuzwa kwake kazi. Alisikitishwa kuwa Tume pamoja na kutambua ukweli huu iliamua kuwa *"ukweli ni kwamba kosa hili halina mashiko, nasema hivyo kwasababu sioni tatizo la mtumishi wa ALAF Limited kumiliki kampuni yake"*

Alibainisha pia kuwa PW1 alitoa utetezi usio na uzito alipoulizwa kuhusiana na mihamala aliyofanya akiwa Arusha kwa jina la Clement Mlanda kwa kusema kuwa "tulitapeliwa na mtu aliyejidai yeye ndie Clement Mlanda". Alisema kwa kuwa mihamala ilifanyika mara nyingi kwa jina la Clement Mlanda PW1 alikuwa na muda wa kutosha kuthibitisha utambulisho wa Clement Mlanda.

Alifafanua Zaidi kuwa, Mjibu Maombi alidangaya kwa wenzake alipotakiwa kutoa ***Bank Deposit slip*** ya Clement Mlanda, aliwaambia Clement Mlana alikuwa mgonjwa sana kiasi cha kushindwa kuitoa na kuwa alikuwa amesafiri kwenda India kwa matibabu na angeweza kutoa hiyo ***slip*** baada ya kurejea nchini. Alibainisha kuwa Mjibu maombi alifanya ulaghai mara nyingi kwa kutumia jina la Clement Mlanda au Kampuni yake ya Ngosero General Supplies Company Limited.

Kwa upande wa hoja (d), (f) na (i) Mleta maombi alielezea kushangazwa kwake na kitendo cha Tume kushindwa kuona kuwa Mjibu Maombi alitumia madaraka yake vibaya kwa kujiuzia bidhaa za kampuni bila kuzilipia.

Alibainisha kuwa Tume ilikataa ushahidi uliotolewa kuwa Mjibu Maombi alitoa Tshs 42,000,000/= kwenye "suspense account" na kukikataa kidhibiti "D7" kinachothibitisha tuhuma hizo kwa kuwa hakikutaja jina la Mjibu Maombi.

Alieleza zaidi kuwa ushahidi mwingine uliodhibitisha tuhuma hizo ni kidhibiti D1, D2, D4, D5, D6 na D7. Na wakati bidhaa zinachukuliwa kwa jina la Clement Mlanda aliyesaini alikuwa ni Mjibu Maombi kulingana na kielelezo D7.

Alifafanua kuwa kielelezo D9 pia kinaelezea kuwa Mjibu Maombi aliuza bidhaa zingine (simba chuma) zenye thamani ya sh 18,326,000/= kwa mkopo kwa kutumia jina la Clement Mlanda. Mjibu Maombi alizipokea bidhaa hizo mkoani Arusha yeye mwenyewe na mpaka wakati wa rufaa hii bidhaa hizo zilikuwa hazijalipiwa.

Alieleza zaidi kuwa, Clement Mlanda (DW5) alikana kuwa hajawahi kufanya biashara yoyote Arusha na hajawahi kufanya biashara na Mjibu Maombi, alikana pia kuwa hajawahi kusafiri kwenda India kwa matibabu. Hivyo, alihoji kuwa endapo Mjibu Maombi hakuwa amehusika na ubadhirifu wa fedha ni kwanini alisema uongo kuhusu masuala hayo. Alisema kuwa, inashangaza kuona Tume haioni tatizo lolote la kumfanya Mjibu Maombi aachishwe kazi.

Aliwasilisha zaidi kuwa Mjibu maombi alitumia makosa ya Mhasibu mwenzake wa Dar es salaam kwenye account ya Clement Mlanda na kuonyesha kuwa Clement Mlanda alinunua bidhaa za shilingi 18,328,311.70 na baadaye kuchukua bidhaa hizo yeye mwenyewe bila kampuni kupata fedha yeyote.

Aliwasilisha pia kuwa ushahidi wa DW1, DW2 na DW12 unaonyesha kuwa Mjibu Maombi aliitumia kampuni yake Ngosero General Supplies Limited kumwibia mwajiri wake. Aliuza bidhaa za mwajiri kwa mkopo kwa

kampuni yake bila ridhaa ya Mwajiri wake huku akijua kuwa hakuruhusiwa kuuza bidhaa kwa mkopo mpaka kampuni inayouziwa iwe imepewa hadhi ya dealer (dealer status) ambayo kampuni yake haikuwa nayo. Kibaya zaidi ni kuwa alikuwa amelimbikiza bidhaa ambazo kampuni yake ilichukua kwa mkopo bila kulipia kufikia kiasi cha TZS 320,658,999/=.

Aidha alieleza kuwa, exhibit D13 inaonyesha kuwa Mjibu Maombi aliingiza taarifa za uongo kwenye vitabu vya kampuni tawi la Arusha ili kumwezesha kufanya mauzo bila kampuni kupokea pesa kwa bidhaa zilizouzwa. Alisema kuwa Mjibu Maombi kwa kutumia nafasi yake kama Mhasibu aliingiza taarifa za uongo kuonyesha kuwa alipokea pesa na kujiuzia bidhaa kupitia katika kampuni yake ya Ngosero General Supplies Limited. Kitendo hiki kilimsababisha Mleta Maombi hasara ya TZS 43 Million.

Alieleza pia kuwa licha ya kwamba Mjibu Maombi hakukataa kutoa bidhaa za mwajiri wake kwa Clement Mlanda, Tume iliamini kisingizio alichokitoa kuwa walitapeliwa na Clement Mlanda. Alibainisha kuwa kwa ushahidi uliotolewa na DW1, DW2, DW3, na DW5 pamoja na kielelezo D1 mpaka D15 Mjibu Maombi alimsababishia Mleta Maombi hasara ya shilingi 424,120,099/=.

Aliieleza kuwa sharia inamruhusu Mleta Maombi kumwachisha kazi Mjibu Maombi kwa makosa aliyoyafanya akiwa kazini. Alirejea kifungu cha 37 (2) cha sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004 pamoja na Guidelines for Disciplinary Incapacity and Incapability Policy and procedures of the Code.

Akizungumzia hoja (h) wakili wa Mleta Maombi aliikosoa Tume kwa kuamua kuwa Mleta Maombi hakufuata taratibu za kisheria katika kumwachisha kazi Mjibu Maombi. Alifafanua kuwa Tume ilibainisha kuwa Mjibu Maombi hakupewa nafasi ya kujitetea kwenye kamati ya nidhamu, hakupewa nafasi ya kujibu tuhuma zinazo mkabili au kuwauliza maswali mashaidi na kupitia nyaraka zilizotumika. Alipingana na uamuzi huu kwa hoja kuwa Mjibu Maombi alipewa nafasi ya kusikilizwa na aliambiwa haki zake kama kielelezo D18 kinavyoonyesha.

Aliendelea kuielezea mahakama kuwa, taratibu zote za kamati ya nidhamu zilifuatwa. Mjibu maombi alipewa hati ya mashtaka, alipewa wito wa kuhudhuria kwenye kikao cha kamati ya nidhamu (kielelezo D18). Baada ya kusikilizwa alipewa nafasi ya kujitetea na aliambiwa ana haki ya kukata rufaa kwa "Chief Executive officer". Alieleza kuwa, mwajiri akishindwa kutimiza vigezo vyote haimaanishi kuwa utaratibu wote umeenda kinyume na sheria. Na wajumbe wa kamati ya nidhamu

walikuwa na sifa kwa kuwa ni waajiriwa kwa zaidi ya miaka 30 kwenye kampuni, hivyo wana uzoefu wakutosha tofauti na anavyosema Mjibu Maombi kuwa walikuwa ni watu wa kawaida.

Akimalizia kwa hoja (c), Wakili wa Mleta maombi aliielezea kuwa Tume ilikosea kwa kuamua kuwa Mjibu Maombi anastahili kulipwa fidia kwasababu ya kuvunjwa kwa mkataba wa kazi. Alifafanua kuwa kwa kuzingatia wingi na ukubwa wa makosa yaliyofanywa na Mjibu Maombi ambayo yalisababisha hasara kwa mwajiri wake na kwa kuzingatia kuwa taratibu za kumwachisha kazi zilifuatwa, Mjibu Maombi hakustahili kulipwa fidia. Alifafanua zaidi kuwa, Mjibu Maombi hakuleta ushahidi wowote kuhusiama na gharama alizodai kama fidia kwenye Fomu namba 1 ya Tume. Kama ilivyoelezwa kwenye kesi ya Marejeo Na. 16/2010, **Sixty Patrick and 2 Others vs The Manager China Paper**, kuwa kabla ya Tume kutoa gharama za fidia lazima kuwe na ushahidi wa gharama hizo.

Akipingana na maombi haya, wakili wa Mjibu Maombi alianza kwa kukosoa kitendo cha Mleta Maombi kuelezea ushahidi uliotolewa na mashahidi Tume kuwa ni kupoteza muda wa mahakama kwa kuwa jalada husika likiitishwa mahakama itapata taarifa za ushahidi uliotolewa. Aidha, alibainisha kuwa katika ukurasa wa 6 wa hoja za Mleta Maombi ameibua hoja mpya ambazo hazikujadiliwa na tume jambo ambalo haliruhusiwi

kisheria. Kama ilivyoamuliwa katika kesi ya **Morandi Rutakyamirwa dhidi ya Petro Joseph** (1990) TLR 49.

Baada ya kueleza hayo alianza kujibu hoja (a), (b) na (e) kama ifuatavyo, kuhusu hoja kuwa DW3 hakuwepo kwenye kikao cha nidhamu, alibainisha kuwa Tume haikukosea kuamua kuwa DW3 hakuwepo kwenye kikao cha nidhamu, alifafanua kuwa kilichomaanishwa na Tume katika ukurasa wa 6, haya ya 2 ya Uamuzi wa Tume ni kuwa wakati wa cross-examination DW3 aliiambia Tume kuwa hakuwepo kwenye kikao cha nidhamu kama shahidi kwenye tuhuma zinazomkabili Mjibu Maombi.

Kuhusu hoja kuwa Tume haikuzingatia ushahidi wa DW4 Clement Mlanda, alieleza kuwa maoni yake ni kuwa Tume haikukosea kutokuzingatia ushahidi wa DW4 kwakuwa DW4 alisema hamfahamu Mjibu Maombi hivyo hawezi kuthibitisha tuhuma kuwa Mjibu Maombi alitumia vibaya mali za kampuni. Hivyo basi, hata kama ilikuwa kweli kuwa Mleta maombi aliathirika kwa kupata hasara kutokana na vitendo vilivyotokea haukuwepo ushahidi kuwa vitendo hivyo vilifanywa na Mjibu Maombi.

Kuhusu ushahidi wa DW5, Adrian Sigalla, alisema kuwa Mleta maombi anajaribu kuidanya Mahakama kwa kusema kuwa DW5

hakufuzwa kwa sababu ya utoro kazini. Alinukuu maelezo ya maelezo ya DW5 katika ukurasa 7 aya ya 1 kuwa:-

> *"...aliachishwa kazi kwa kosa la kutokuwepo kazini, kufanya biashara inayofanana na ya mwajiri wake kwa kutumia kampuni yake ya Ngosero bila kusema..."*

Kwa maoni ya Mleta Maombi, haoni kuwa kuna makosa yoyote yaliyofanywa na Tume kwa kitendo cha kunukuu kilichosemwa na shahidi wakati ikichambua ushahidi ulioletwa Mahakamani.

Aidha, kuhusu hoja kuwa Mjibu Maombi alikosea kwa kuuza bidhaa za mwajiri kwa mkopo bila kibali cha mwajiri, alisema kuwa anakubalina na uamuzi wa Tume kuwa maelezo hayo "hayana mashiko" kwa kuwa Kanuni za Uendeshaji wa Kampuni (Business Code of Conduct) za Mleta Maombi zilifikishwa kwa Mjibu Maombi mwaka 2017 baada ya kuwa kampuni ya Mjibu Maombi imekwisha sajiliwa na BRELA tangu mwaka 2012 na kuanza kazi.

Kuhusu tuhuma za kujiuzia bidhaa zenye thamani ya Shilingi 320,658,999/= kwa mkopo, alibainisha kuwa Tume haikujihusisha na tuhuma hizi kwa kuwa hili ni suala la madai ya kimkataba kati ya Mleta Maombi na kampuni ya Mjibu maombi ambalo haliko kwenye mamlaka ya Tume.

Kuhusu tuhuma kuwa Mjibu Maombi alijihusisha na vitendo vya kihalifu kama kujaza taarifa za uongo kwenye vitabu vya benki na kujipatia fedha kwa njia udanganyifu, alibainisha kuwa hizi ni tuhuma za kijinai zinazopaswa kudhibitishwa na mamlaka husika kabla ya kumchukulia hatua mtumishi husika. Alirejea kifungu cha 37(5) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004 katika kuimarisha hoja yake. Hivyo basi, aliona kuwa Tume ilikuwa sahihi kuamua kuwa Mleta maombi alimwachisha kazi Mjibu Maombi pasipokuwa na sababu za msingi na pasipokufuata utaratibu.

Kuhusu hoja kuwa Tume ilimtetea Mjibu Maombi katika tuhuma za matumizi mabaya ya ofisi kama ilivyoelezwa katika hoja (d), (f) na (i), alijibu kuwa Tume haina mamlaka ya kisheria ya kusikiliza tuhuma za matumizi mabaya ya ofisi hivyo, isingekuwa sawa kwa Tume kufanya uamuzi katika masuala ya kijinai kama suala hili. Hivyo basi, Tume ilikuwa sahihi kuachana na hoja hiyo na kuamua kuwa hakuna tatizo kwa mwajiriwa kumiliki kampuni yake binafsi.

Kwa upande wa hoja (h), alieleza kuwa, Tume ilikuwa sahihi kuamua kuwa utaratibu wa kikao cha nidhamu haukufuatwa kutokana na upungufu uliojionyesha. Alisema kuwa, mashahidi wa muhimu hawakuhudhuria kikao hicho kuthibitisha tuhuma zilizotolewa dhidi ya

Mjibu Maombi akiwepo aliyeandika barua ya kumwachisha kazi Mjibu Maombi. Alitoa maoni yake kuwa, Mleta maombi alitafsiri vibaya uchambuzi uliofanywa na Tume kwa kuwa katika ukurasa wa 12 mpaka wa 14 wa uamuzi wake, Tume ilibanisha kuwa wakati wa kikao cha maadili kulikuwa na kasoro za msingi na ukiukwaji wa sheria katika utaratibu mzima wa kumwachisha kazi Mjibu Maombi. Kwanza, ushahidi unaonyesha kuwa wakati wa kikao cha maadili Mleta Maombi hakumuita mtu yeyote kama shahidi, taarifa ya upelelezi inayoonyesha kuwa Mjibu maombi alihusika katika masuala aliyotuhumiwa kuyafanya haikutolewa katika kikao cha maadili ili kuthibitisha ukweli wa madai hayo. Pili, haikuwa sahihi kwa Daphne Kakonge kumwandikia Mjibu Maombi barua ya kumwachishwa kazi wakati hakuwa sehemu ya kikao cha maadili na hivyo hakuwa na uelewa wa mambo yaliyojiri katika kikao cha maadili.

Aidha, kuhusu hoja kuwa wajumbe wa kikao cha maadili walikuwa ni wafanyakazi wa kawaida wa kampuni ya ALAF, alisema kuwa hoja hii si ya kweli kwa kuwa suala hilo halikuzungumzwa popote katika uamuzi wa Tume.

Kuhusu hoja ya mwisho (c) ambayo ilieleza kuwa Tume ilikosea kuamua kuwa Mjibu maombi anastahili kulipwa fidia kwa kuvunjwa kwa mkataba, wakili alielezea kuwa, malalamiko ya Mjibu Maombi katika CMA

F1 talikuwa yanahusu kuachishwa kazi pasipo kufuata taratibu za kisheria na sio kuvunjika kwa mkataba kama alivyodai mleta maombi. Alifafanua kuwa Tume ilikuwa sahihi kutoa fidia ya Miezi 36 kwa kwa kitendo cha kuachishwa kazi kinyume cha sharia chini ya kifungu cha 40 (1) (c) cha sheria ya Ajira na Mahusiano kazini, 2004. Kifungu hicho kinaruhusu mtumishi aliyeachishwa kazi bila kufuata taratibu za kisheria kulipwa fidia kuanzia miezi 12. Alieleza kuwa, hakuna haja ya kuthibitisha fidia hizo kwa kuwa zipo kwa mujibu wa sheria. Hivyo, aliiomba mahakama ikubaliane na uamuzi ya Tume katika shauri hili.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili na kupitia kumbukumbu za shauri hili, kwa kuzingatia hoja zilizoletwa na Mleta maombi, mahakama hii inaona kuwa maombi haya yanaibua masuala matatu ya msingi yanayostahili kutafutiwa ufumbuzi, ambayo ni: Kwanza, kama Mleta Maombi alikuwa na sababu za msingi za kumwachisha kazi Mjibu Maombi; Pili, kama Mleta Maombi alifuata utaratibu wa kisheria katika kumwachisha kazi Mjibu Maombi; na tatu, ni nafuu zipi zinazostahili kutolewa kwa wadaawa katika shauri hili.

Nikianza na hoja ya kwanza, kama Mleta Maombi alikuwa na sababu za msingi za kumwachisha kazi Mjibu Maombi. Kulingana na barua iliyomwachisha kazi Mjibu Maombi (exh D20), Mjibu maombi aliachishwa

kazi baada ya kupatikana na hatia ya kufanya makosa matatu ambayo ni ***Gross dishonesty, Loss of integrity*** *na* ***misuse of office for personal gain.***

Kuhusu kosa la ***Gross dishonesty***, hati ya mashtaka (D17) na muhtasari wa kikao cha nidhamu (D19) unaonyesha kuwa tuhuma dhidi ya Mjibu maombi ni kuwa Mjibu maombi hakumtaarifu mwajiri wake kuwa ni mmiliki wa kampuni ya Ngosero General Supplies Limited ambayo ni dealer wa kununua bidhaa kutoka kwa mwajiri wake kinyume cha business code of conduct inayomtaka kumtaarifu mwajiri wake kuhusu maslahi aliyonayo kwa wateja wanaofanya biashara na mwajiri wake. Hata hivyo, mwajiri hakutaja kanuni au kipengele mahsusi cha Business Code of Conduct kilichotamka hivyo. Kulingana na muhtasari wa kikao cha nidhamu (hearing form), ushahidi uliotolewa na mwajiri kuthibitisha kosa hili ni pamoja na: Nyaraka kutoka kwa Msajili wa Makampuni (BRELA) kuonyesha kuwa Mjibu maombi ni mmiliki wa Ngosero General Supplies Limited; Sera ya Kanuni na Miiko ya Kibishara (Business Code of Conduct Policy); Mahudhurio ya mafunzo kuhusu kanuni na miiko ya kibiashara; na ushahidi kuwa mwajiriwa hakutoa taarifa kuwa ni mmiliki wa Ngosero General Supplies Limited.

Uamuzi wa rufaa iliyopelekwa kwa uongozi wa mwajiri ulibainisha kuwa mwajiriwa hazuiliwi kuwa na kampuni ila ni makosa kwa mwajiriwa kuacha kumtaarifu mwajiri kuwa ni mmiliki wa kampuni inayofanya biashara na mwajiri wake.

Mahakama hii kwa kuzingatia kuwa hati ya mashtaka (D17) na muhtasari wa kikao cha nidhamu (D19) havikutaja ni kanuni ipi au kipengele kipi cha Business Code of conduct kilichovunjwa na Mwajiriwa, inaona kuwa mwajiri hakuweka bayana kosa lililofanywa na mwajiriwa ili kumruhusu mwajiriwa kuandaa ushahidi wake wakati wa kikao cha nidhamu na mbele ya Tume. Maelezo kuwa mwajiriwa alikiri kuwa hakutoa taarifa za umiliki wa kampuni ya Ngosero au kuwa alihudhuria mafunzo kuhusu kanuni na miiko ya kibiashara hayatoshi kutengeneza sababu ya kumwachisha kazi mwajiriwa bila ya kubainisha kanuni au kipengele mahsusi cha Kanuni na Miiko ya Kibishara anachotuhumiwa mwajiriwa kukivunja. Hivyo basi, mahakama hii inaona kuwa mwajiri alishindwa kuthibitisha sababu ya kumwachisha kazi mwajiriwa katika kosa hili.

Kuhusu kosa la Loss of integrity, hati ya mashtaka inaonyesha kuwa tuhuma dhidi ya mwajiriwa ni kuwa alimdanganya mwajiri wake kwa kuruhusu mauzo ya bidhaa kwa jina la Clement Mlanda kwa udanganyifu

na hivyo kumsababishia mwajiri wake hasara ya Shilingi 60,321,200/=. Hati ya kiapo ilibainisha kuwa, mwajiriwa kwa kujifanya anamfahamu Clement Mlanda na amepata fedha kiasi cha Shiling 42,000,000/= alihamisha kiasi hicho cha pesa kwa jina la Clement Mlnda kutoka kwenye suspense account (unexplained bank credit). Baada ya fedha hizo kuhamishwa aliruhusu mauzo ya Shilingi 23,671,650/= tarehe 9/9/2017 na shilingi 18,326,850/=, jumla ikiwa shilingi 41,998,500/= dhidi ya deposit ya shilingi 42,000,000/=. Baada ya uchunguzi uongozi wa kampuni ya mwajiri ulibaini kuwa Clement Mlanda anafanya biashara kwa jina la Mlashi General Traders na fedha kiasi cha 42,000,000/= ni za Mlashi General Traders na kuwa hakufanya biashara na tawi la mwajiri la Arusha. Aidha, hati ya mashtaka ilibainisha pia kuwa mwajiriwa aliruhusu mauzo mengine ya shilingi 18,322,700/= bila kupokea malipo na kuingia kwenye mfumo wa fedha kwa kutumia utambulisho wa mtu mwingine kubadilisha maingizo kwenye mfumo.

Ushahidi uliotolewa katika kamati ya nidhamu kuthibitisha kosa hili ni: barua pepe ya Finance Manager ya tarehe 27/7/2017; maelezo kuwa mwajiriwa kwa kutumia utambulisho wake (user identity) alifungua akaunti kwa jina la Clement Mlanda (project customer); barua pepe mbalimbali zikimuonyesha mwajiriwa kama mwanzilishi akiomba kibali

cha kuhamisha fedha kutoka makao makuu ya mwajiri wake kwenda Arusha kwenye jina la mteja Clement Mlanda; hati za malipo zilizoonyesha namna malipo yaliyovyofanyika ambayo mwajiriwa alishiriki; na barua kutoka kwa Clement Mlanda mwenyewe aliyepo Mwanza akikana kufanya biashara na tawi la mwajiri la Arusha.

Katika utetezi wake mwajiriwa alibainisha kuwa katika mihamala iliyotajwa na mwajiri taratibu za kupata idhini (approval) zilifuatawa na Meneja wa Fedha pamoja na Meneja wa tawi walipewa nakala ya kila muhamala; kwamba mwajiriwa pamoja na Meneja wa tawi kwa pamoja wamewahi kukutana na mteja mwenye jina la Clement Mlanda akiwa amekuja kwenye tawi la Arusha.

Mahakama hii, kwa kuzingatia ushahidi ulioletwa mbele ya Tume kuthibitisha kosa la mwajiriwa, inaona kuwa kwa kuzingatia aina ya tuhuma dhidi ya mwajiriwa, ilikuwa ni lazima kwa Mwajiriwa kupewa taarifa ya uchunguzi (investigation report) inayoonyesha namna uchunguzi unavyoonyesha uhusika wake katika tuhuma husika ili kumwezesha kujiandaa na utetezi wa tuhuma dhidi yake. Ushahidi unaonyesha kuwa taarifa ya uchunguzi haikutolewa kwa mwajiriwa wala mbele ya kamati ya nidhamu. Aidha, Clement Mlanda ambaye jina lake inasemekana lilitumiwa mara nyingi na mwajiriwa kujipatia bidhaa kutoka

kwa mwajiri kwa njia ya udanganyifu hakuhudhuria kwenye kikao cha nidhamu kuithibitishia Kamati tuhuma hizi ingawa barua inayosemekana aliindika kuthibitisha madai haya ilitumiwa na Kamati katika kufanya maamuzi yake na mwajiriwa hakuwa na nafasi ya kumuuliza maswali kuhusiana na barua hiyo. Hivyo basi, mahakama hii inaona kuwa Kamati ilifanya uamuzi bila kupata ushahidi wa kutosha kuthibitisha tuhuma dhidi ya mwajiriwa. Katika mazingira haya, mahakama hii haimini kuwa sababu ya kumwachisha mwajiri kazi ilithibitishwa kwa kiwango kinachotakiwa.

ushahidi uliotolewa mbele ya Tume unaonyesha kuwa Mjibu Maombi aliachishwa kazi kutokana na matumizi mabaya ya ofisi ambayo ni pamoja na kuikopesha kampuni yake binafsi ya Ngosero General Supplies Limited bidhaa kutoka kwa Mwajiri wake kinyume na taratibu za kampuni na bila kibali cha mwajiri, kutumia vibaya jina la Mteja wa mwajiri wake, Clement Mlanda na kujipatia bidhaa kwa udanganyifu pamoja na kujaza taarifa za uongo kwenye vitabu vya benki vya kampuni ya mwajiri wake. Mahakama inaona kuwa upungufu huu unahusika pia katika kosa la misuse of office for personal gain.

Hoja ya pili inahusu kufuata taratibu zilizoanishwa kisheria wakati wa kumfukuza mwajiriwa. Tume ilibaini kuwa baadhi ya taratibu

hazikufuatwa na hivyo uamuzi wa kumwachisha kazi mwajiriwa ulikiuka taratibu za kisheria. Kwa mujibu wa Kanuni ya 13 ya G.N. Na. 42/2007, mwajiri anatakiwa kufuata kanuni zilizoainishwa katika kumwachisha kazi mfanyakazi wake. Mahakama hii inakubalina na Tume kuwa kwa kuzingatia makosa aliyotuhumiwa nayo mleta maombi kulikuwa na ulazima wa kufanyika uchunguzi na ripoti ya uchunguzi huo kutumiwa na kamati ya nidhamu katika kufanya uamuzi wake kama inavyoelekezwa katika kanuni ya 13 (1) ya G.N. Na. 42/2007. Kukosekana kwa taarifa ya uchunguzi ambayo Mahakama hii inaona kuwa kuwa ilikuwa na umuhimu mkubwa katika kuthibitisha makosa dhidi ya mwajiri ni dosari kubwa inayoonyesha namna ambavyo mwajiri hakufuata utaratibu wa kisheria katika kumuachisha kazi mjibu maombi kama inavyotakiwa.

Kuhusu nafuu zinazostahili kutolewa na mahakama, baada ya kupitia hoja za pande zote mbili pamoja na fomu ya lalamiko iliyowasilishwa mbele ya Tume (CMA Form No. 1) ambayo inaonyesha kuwa mwajiriwa aliomba pamoja na vitu vingine fidia ya miezi 36 kwa kuachishwa kazi isivyo halali, Mahakama hii kwa kuzingatia mazingira ya kesi hii na ushahidi uliotolewa na pande zote inaona kuwa nafuu ya fidia ya mishahara ya miezi kumi na mbili (12) chini ya kifungu cha 40 (1) (c) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004 inastahili katika mazingira

ya kesi hii na ni uamuzi wa Mahakama kuwa Mwajiriwa alipe hivyo. Aidha, mwajiriwa anastahili pia kulipwa haki zake za kuachishwa kazi chini ya kifungu cha 44 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, 2004 iwapo haki hizo hazikulipwa wakati wa kuachishwa kazi.

K.N.ROBERT
JUDGE
22/9/2021